**BARUA WAZI LA MSAMAHA KWA DUNIA (OPEN LETTER OF APOLOGY TO THE WORLD)**

Tafadhali nivumilie. Muda mrefu umepitwa na kuna mambo mengi ya kuzungumzia. Nataka kuhakikisha ya kwamba nimeyasema yote. Siyo kwa ajili yangu pekee, lakini nafikiri wewe unahitaji kuyasikia pia. Labda kuna Wakristu wengine huko nje pia, ambao wanahitaji kusema pole na watapata ujasiri (courage) hapa. Nakushukuru kwa muda wako, najua ni ya dhamana sana.

**Wapendwa wa dunia,**

Mimi ni mtu tu, si kitu kweli. Mimi ni mwana wa Mhubiri na Mmishonari. Nilipokuwa kijana, nilifanya miaka na miaka ya masomo ya Bibilia wakati wa likizo (Bible School), pia nilienda Makambi wakati wa majira za joto (Summer camps), pia nilihudhuria Maonyesho ya vikaragosi (puppet shows), Viamsho (revivals), na pia nikasafiri na makwaya. Hata nilienda chuo cha Ukristu na nikapata shahada (degree) ya dini. Halafu nikaenda kwenye dunia la biashara nikichukua miaka ishirini nikipeana sadaka, nikiketi kwenye makamati, nikifunza Shule ya watoto ya Jumapili (Sunday school), nikienda kwenye masemina na mikutano na kadhalika. Hata nilikutana na aliyekuja kuwa mke wangu kanisani, kwenye darasa la wale hawakuwa wameoa. Mimi si mtu mbaya, sanasana nimekuwa na tabia nzuri na kila mtu anakaa kunipenda. Mimi huwa nafanya vitu vizuri hapa na pale.

Lakini hivi majuzi, nimekuwa nikijaribu kumuelewa YESU zaidi, na vitu ambavyo sikuwa nimeviona mbeleni vimeanza kuniudhi. Nimekuwa nikiangalia kote na nimepata wakati mgumu kuelewa ni nini tumeijenga hapa. Kwa hivyo, mtu asipolisema au aliseme, ninahitaji kuchukua wajibu (responsibility) kwa lile jukumu (role) nililofanya, na niyasema ninayofaa kuyasema.

Haya, tuende basi,

Najua unadhania wakristu ni wanafiki (hypocrites). Tunashinda tukisema tuko na ‘ udini ’ (religious) zaidi ya wengine na eti tunaenda mbinguni na eti wewe huendi, halafu tunayaendesha magari yetu mazuri na kukupita kwenye trafiki, saa hizo tukimpita maskini aliye kando ya barabara ambaye hana makazi. Huwa tunapeana 2% ya pesa zetu kwa kanisa na hisani (charity), huku tukisema ya kwamba Bibilia ni NENO LA MUNGU na linasema tunafaa kupeana kila kitu. Kwa wastani (average), tunayanunua matelevisheni na mashua (boats) makubwa na makoti ya manyoya (fur coats) na vipodozi (make-up) na sinema za ngono (porn) kama tu watu wengine. Labda zaidi. Umemuona kiongozi baada ya kiongozi akipelekwa gerezani au mahakamani kwa ajili ya kashfa (scandal) moja au lingine.

Kweli, hujakosea. Tuko na hatia kwa haya mambo yote kwa sababu tumeyafanya. Na, ninasema pole.

Unaziona maprogramu (Televangelist programs) zetu za televisheni ambazo zina watu ambao wanaomba pesa na unaweza ona ziko na mambo mabaya. Watu kwenye hizi maprogramu wanaitisha pesa kwa uzito mno ili maprogramu zao ziweze kubaki kwenye televisheni. Ni nani

tunadhani tunadanganya?! YESU yuko wapi ndani ya haya yote?! Si tunapaswa kumtegemea? Si atatupatia mahitaji yetu kama tuko ndani ya matakwa YAKE?

Ni nini iliyofanyikia kujitolea na kuteseka na kuwasaidia masikini? 'Nimegonjeka' kwa kuona haya. Simaanishi eti ni viongozi wote wa kanisa wabaya, kunao wengi sana ambao wanafanya kazi nyingi sana na wanawajali na kuwapenda na kuwasaidia wale ambao wako na mahitaji. Wengine wao wanampenda na kumuelewa YESU – Lakini niko na uhakika ya kwamba, mapasta kama hao hawaendeshi magari makubwa, hawana manyumba makubwa yenye dhamana ya $5 milioni na mandege. Ni mungu mgani ambaye tunayemuabudu?! Pesa?! Kiburi?! Nguvu?!

Unayaona manyumba yetu kila mahali yanayo meta meta. Labda hata tulikufukuza kutoka kwa nyumba yako ili tuweze kuongeza nafasi ya kuyaweka magari yetu. Ni vigumu kuelewa mbona tunayahitaji makanisa tofauti ambayo yako sehemu moja. Tuko na viwanja vya watoto kuchezea na viwanja vya mpira wa kikapu. Tuko na mahali za kukunywa kahawa ndani ya makanisa (Starbucks). Tuko na uchezaji mziki na umaridadi wa mataa mbele ya makanisa. Tuko na maduka ya vitabu ambayo yamejaa 'mambo ya YESU' na madoido mengi. Lakini nauliza, YESU yuko wapi katika haya yote?! Ni haya kweli aliyokuwa anayataka?

Kwa uhakika, kunao watu wazuri kwote na siyo kila kanisa liko na fujo. Lakini wakristu ni wale wanaosema wao ni 'Mwili Mmoja'(One Body)**.** Kwa hivyo, hata wale wazuri wako na hatia ya kutosimamisha haya mambo mabaya mapema. Tunafaa tuwekane laini na tusivumilie migawanyiko na kutokubaliana, na ulafi na ibada ya sanamu na haya mambo mabaya. Waah! Kweli tulikosa. Tukona migawanyiko au madhehebu (denominations) 33,000 na mingi zao haziwezi ongeleshana. Tunapoteza $5milioni kutokana na watu waliyo ndani ya kanisa ambao 'wameaminika'. Tunatumia 95% ya pesa yetu kwa ustarehe na maprogramu zetu na tunawaacha wakristu 250 milioni wa nchi zingine wakiishi wakiwa njaa. Na hata hatujataja mabilioni ya watu ambao hawajasikia kumhusu YESU – au yule maskini ambaye hana makao, mwenye karibu akanyagwe na gari barabarani.

Sisi tukona hatia. Sisi sote. Hakuna ambaye ameepuka. Tulikuwa tunapaswa kuweka kikomo kwa haya maneno, mapema zaidi. Lakini siwezi sema pole kwa niaba ya mtu mwingine. Hii ni juu yangu.

Najua unaweza kuwa ulikuwa unaenda kanisani ukiwa mtoto na ulipoweza kuacha kuenda, ukaacha. Najua unaweza kuwa ulinyanyaswa na mtu wa kanisa! Labda tulikutia moto, halafu tukakuwacha upotee ni kama hatukukujali. Labda hukuwa 'unakaa kama sisi'. Unaweza kuwa umetoboa masikio, mapua au ulimi. Unaweza kuwa umeweka rangi ya zambarau kwenye nywele pia au ukona tattoo au umekuwa gerezani – na ndani yako unajua ya kwamba kama ungetaka kuenda kanisani Jumapili moja, mambo hayangeenda sawa. Pole kwa hayo. YESU anakupenda, alikuwa anashinda akikaa na wale ambao hungetarajia. Alikuwa na ROHO kubwa kwa wale waliokuwa wamepuuzwa. Ni nini tumefanya? Tumekwambia eti uvae sweta na 'loafers' (viatu virembo) au hautaweza kuenda mbinguni. Nataka tu kutapika nikiskia haya.

Ona, najua umekasirika. Na ukona na haki ya kukasirika. Tumewakosea kwa muda mrefu sana. Kuna vitu kumhusu YESU ambavyo watu wanahitaji kuvisikia, lakini tumeizika neno nzuri chini ya 'rangi nyingi nyororo'. Kama uko na bibilia, enda kwenye Mathayo 23 (Matthew 23). (Kama huna bibilia, enda kwenye www.BibleGateway.com). Umeipata? Soma kwa utaratibu, mafarisayo (pharisees) ndiyo waliyokuwa 'wenye dini' siku hizo, waongozi wa Imani. Kwa hili Sura, YESU anasema mara saba vile wao ni wa kusikitisha, ni wanyonge na wamelaaniwa kwa sababu ya yale wanayotendea wafuasi wao. Hata anawaita 'makaburi yaliyopakwa chokaa yenye mifupa ya walioaga' (tombs of dead mens' bones). Na pia akawaita 'Kizazi cha nyoka' (brood of vipers). Sina wakati saa hii, lakini isome na uone kama hatuvifanyi vitu hivyo. YESU hawezi kuwa amefurahi nasi kwa tulichowatendea waliyo kwenye dunia (those in the 'world').

Na Kweli, tunapenda kujidanganya na kujifanya ya kuwa kila kitu kiko sawa. Lakini hakiko sawa. Tunachukiwa. Lakini elewa pia ya kwamba YESU alichukiwa pia, kwa sababu alisema maneno magumu na wakati mwingine, watu hawapendi kuisikia UKWELI. Na aliahidi ya kwamba tukiwa kama YEYE, tutachukiwa**.** Lakini wakati huu, hatuchukiwi na 'waliyo kwenye dunia' (the unsaved in the world) kwa hilo sababu. Tunachukiwa kwa sababu sisi kama Wakristu ni waongo na wanafiki (hypocrites). Tunalisema kitu kimoja halafu tunalitenda kingine. Kama tungelichukiwa kwa sababu ya kuwa kama YESU, hicho kingekuwa kitu kingine lakini siyo hivyo. Nyinyi 'mliyo kwenye dunia', mnaeza ona kwa kupitia 'miziki zetu za furaha' na 'huduma zetu nzuri ' ya kwamba kuna kitu ambacho hakiko sawa. Hatuna utofauti na wengine – ila tu tunasema 'tuko sawa kuwaliko'.

Haikufaa kuwa hivi. YESU alituambia tuwajali wajane na mayatima, kuwalisha wenye njaa, kuwajali wagonjwa, kuwatembelea waliyo gerezani na kuwahubiria 'waliyopotea'. YEYE KRISTU alitaka tuwapende maadui zetu na tuwaombee. Akijali kuhusu haki ya binaadamu na mateso yao na pia wale hawakuwa ndani YAKE (KRISTU) na pia wale waliokuwa wanakaa pekee yao bila ya mtu kuwajali. Lakini sidhani kama angetembea kwenye laini ya mpaka**.** AKILI YAKE ilikuwa kwenye mashida makubwa. ALIKUWA anataka tuzingatie vitu vya milele (eternal things), sio vitu vya kila siku. Hakuwai sema, tuende kwenye dunia tujenge manyumba makubwa ya kanisa na kugawanya kanisa na kuzinunua magari yenye dhamana kubwa. Tunapaswa kufanya kinyume cha hayo. Naelewa umeikasirikia kanisa, na uko na haki ya kuikasirikia, lakini tafadhali elewa, umeikasirikia kitu tulichokitengeza kwa 'nguvu' yetu; umeikasirikia 'ukanisa'. 'Ukanisa'(Churchianity) uko na utofauti na KRISTU alichotaka. Usimkasirikie KRISTU! Huu uovu haukuwa mpango WAKE.

Mimi ninasema pole, Ninakubali ya kwamba nimekukosea kwa kukuumiza. Lakini ninajitolea kwenu nyinyi wakristu wote duniani nikisema, sitaendelea kuwakosea tena. Sitaendelea kuweka Imani yangu ndani ya 'ukanisa', kiongozi yeyote au programu au kipindi chochote televisheni, ila tu kwa YESU KRISTU na Uokovu WAKE. Hapo ndipo nilipoanza kuachiliwa huru na nikaanza kuona kwamba, MUNGU anataka na anatarajia mengi Zaidi kutoka sisi kuliko haya. Na simsaidii yeyote ambaye hajajitolea kwa mambo haya pia.

Imechukua miaka mingi kuyajenga haya maovu, kwa hivyo siyo eti yataisha kwa siku moja. Lakini nyakati zinabadilika na tumeshapita muda wa kitu kipya. Mambo mabaya yanatendeka- kama ile tsunami iliyotendeka bara la Asia – na nafikiri kunazo zingine zinaja. Mimi sitaki muda mwingine upite bila mimi kusema haya. Mimi nasema pole kwa ule muda na pesa nimepoteza. Lakini KRISTU anaokoa. Kabisa. Kanisa yenyewe hata siyo yenye kuzingatia sana. KRISTU ni MKWELI kabisa. YEYE aliishi na akafa kwa ajili ya dhambi zetu halafu akafufuka tena . YEYE ni YULE aliyesema ALIKUWA na anawajali mimi na wewe. YEYE ni MTUMAINI wetu wa pekee (HE IS our only hope). Tunahitaji mahali nyingi tunazoweza kuenda kufunzwa kuhusu KRISTU na iwe mahali ambapo huta yumba yumba au kujaribiwa au kuzuiwa na kitu kingine. MUNGU akipenda, mahali kama hizo zitakuja kuwa.

Tafadhali usifikiri ya kuwa, wakristu wote si wa ukweli. Wengine wao hawadanganyi wanaposema wao ni wakristu. Shida ni kuwa, sana sana huku Magharibini (in the West, mostly America), sisi tunapenda ustarehe na tunapenda ibaki hivyo. Wakristo waliyo nchi ya Uchina na nchi zingine wanaichukulia ukristu wao kwa umakini sana na hawaichezei. Wanapowatoroka wafanya kazi wa serikali, hakuna nafasi cha kitu kingine ila YESU. Wanakufa kila siku kwa ajili ya Imani yao, na wanavifanya vitu vigumu kwa sababu wamejitolea kumtumikia KRISTU. Wao ndiyo wale waliyo tayari kumfia KRISTU. Wao ndiyo wale waliyo tayari kuzisulubisha sehemu ndogo za maisha zao kila siku, ili waweze kukukaribia kuwa kama KRISTU zaidi na zaidi. Wako tayari kuyaweka mambo yote ya maisha yao kando, ili waweze kufanya kile KRISTU anachokitaka. Wako tayari kuozea gerezani au kuchukua kichapo, au kufa kama hivyo ndivyo inavyotakikana. Hawa wakristu wanatenda kwa upendo msafi na hawarudi nyuma. Mimi mwenyewe sitoshi dhamana ya kuzifunga kamba za viatu vyao. Hapa nilipo muda huu, kunao kama hao pia, na nina matumaini tunaweza kuwaanzisha watu kuishi hivyo. Muda tayari umechelewa zaidi.

Kama unamuongelesha mtu anayesema yeye ni mkristu, muulize kama yeye ni mkristu kila mara au ni mkristu siku ya Jumapili peke yake. Bibilia inasema, tutawajua kwa ‘matunda’ yao (we will know them by their fruits) – kwa Imani na usafi na upendo ndani ya vitendo na maneno yao. Utakapo mpata mmoja anayedhibitisha KRISTU yuko ndani yake, kwa vile anavyokupenda, muulize akueleze kumhusu KRISTU. Kama unamjua mmoja wa wale waliyo tayari kumfia YESU, ambaye hana uoga, ambaye anaongea ‘maneno magumu’ – masafi yenye ukweli – muulize maswali mengi. ‘UKWELI’ uko kwa uchache kuliko unavyofikiria. Lakini usitulie ndani ya ‘ukweli mnyororo’, yenye ustarehe – ukweli kama huo, hauko kwenye bibilia.

Tutajaribu kuwaita pamoja waliyotayari kumfia YESU na kuanza kufanya yale KRISTU aliyoyataka. Kama nitakutana nawe siku moja, nitaomba unipe mkono wako nikusalimie na nikuombe msamaha. Nitajaribu zaidi kutoka sasa, ninaahidi. Nafikiri kuna wengi wengine ambao wanakubaliana nami. Kwa hivyo, usishtuke kama utaanza kuviskia vitu kama hivi.

Asante kwa muda wako. Nina matumaini itasadia.

**Doug Perry – Mji wa Kansas, Missouri, USA**
www.fellowshipofthemartyrs.com - fotm@fellowshipofthemartyrs.com - www.youtube.com/fotm1